UBAINIFU YAKINIFU

(kuhusu makosa ya kimanhaji na kielimu, yaliofanywa
na baadhi ya wanaojinasibisha na maswala ya elimu)

MAKALA NO (9)

IMEANDIKWA NA:

ABUU IBRAAHIIM IBNU AL IMAAM

١٤٣٨/٤/٢٢هـ

بسم الله الرحمن الرحيم.

الحمد لله رب العالمين، والصلاة والسلام على النبي الكريم، وعلى آله وأصحابه أجمعين.

أما بعد.

Baada ya kumshukuru Allah Mtukufu, na kumswalia Mtume wetu kipenzi, na Ahli zake, na Maswahaba wake wote:

Ndugu msomaji, ni wakati mwingine wa kueleza baadhi ya mambo yasio ya kielimu yaliyofanywa hasa na Khamis Ame.

Bila kupoteza muda mwingi, naingia moja kwa moja kwenye maudhui, nayo ni swala la wakati mwingine mlinganizi au Shekhe kukosea lafdhi ya Hadithi au kukosea jina la mpokezi wa hadithi au kusahau kipande cha Aya na mfano wake.

Vitu hivi ni vya kawaida sana kwa walinganizi, bali hata kwa mashekhe wakubwa baadhi ya wakati hutokea, kwani hakuna mkamilifu zaidi ya Alla, na wala hicho si kipimo cha kumdharau mtu na kumkejeli.

Maana ingekua hicho ndicho kipimo, basi

tungewadharau mashekhe wengi sana,kwani tunashuhudia kwenye Ufundishaji wao hutokea baadhi ya wakati akapatwa na waham akataja kitu kimakosa, kisha kesho yake anakuja kusahihisha, au inatokea mwanafunzi kumtanabahisha, na hilo ni swala la kawaida sana kwenye elimu.

Bali imetokea huko zamani baadhi ya maulamaa kuandika vitabu vya kuwasahihisha baadhi ya wanachuoni wa hadithi waliokosea kwenye baadhi ya matamshi ya hadithi na kadhalika.

Lakini cha kushangaza na kutia huruma sana kwa khamis Ame na mfano wake: kwao wao mlinganizi asiyekua wao akikosea kidogo tu kwenye Aya au lafdhi ya hadithi au mpokezi au matamshi ya ibara flani, basi ni vigelegle na kushangilia, na kwamba huyu mwenye kukosea hana akili wala hana analojua na ni mjinga na mpumbavu!

Kwa hakika huu si mwenendo wa kielimu, na ni ujaahili ambao wanachuoni wameukemea.

Amesema Al Imaam **Rabi'I** bin Haady Al madkhaly Alla amhifadhi:

"الآن في الساحة أصناف من هذا الشكل، الإنسان إذا أخطأ خطأ واحدا أو جهل مسألة قالوا: والله جاهل! هذه المناهج هدامة، يجب أن نحترم العلماء، وأن نحترم طلاب العلم، وأن يحترم المسلمون بعضهم بعضا، وألا نستحل الأعراض بأقل فرصة تجدها تنتهزها للنيل من أخيك المسلم".

مرحبا يا طالب العلم ص: ٣٤٢.

"Sasa hivi kwenye uwanja (wa da'wa) kuna watu mfano huu, (ambao wana mtazamo kua)mtu akikosea kwenye kosa moja, au asipojua mas'ala flani, wanasema: "waLLaahi ni mjinga"!.

Hizi ni manhaji mbovu, lazima tuwaheshimu wanachuoni, na tuwaheshimu wanafunzi, na Waislamu waheshimiane wao kwa wao, na tusihalalishe heshima za watu kwa fursa ndogo unayoipata ukaitumia kwa ajili ya kumvunjia heshima ndugu yako Muislamu"

Tazama: marhaban yaatwaalib Ilmi uk: 342.

Lakini huenda hawa watu waliiga tabia hii kutoka kwa baadhi ya wenzao, kwani wako waliyokua wakiwafanyia maulamaa wakubwa wa Ahlu Ssunna wal jama'a kama hivyo, wakatahadharishwa na

kuonywa ila hawakusikia!

Lakini ilipotokea baadhi ya mashekhe kubainisha makosa ya Shekhe wao Yahya Al hajuri kua hata yeye ana makosa tena kuzidi ya wengine: ndipo baadhi yao wakaanza kuachana na tabia hiyo.

Bali mmoja katika wao kupitia website yao ya ya al uloom (katika harakati zake za kumtetea Hajury) ametolea dalili na Shekhe Ahmad Annajmy Allah amrehemu kuwa amewaraddi watu wa bida'a ambao wanafuatilia makosa kama hayo na kuacha maswala muhimu ya kielimu.

Yani huyu kwenye huu mtandao amesema hayo akiwa ana mjibu mmoja miongoni mwa vijana waliokua wanataja makosa ya Yahya Al Hajury katika maswala ya uandishi, na lugha na n k.

Lakini cha kushangaa ni hawa wenzao wa huku Tanzania, ambao hawajawaidhika, si na maneno ya maulamaa wetu wakubwa, au maneno ya mwenzao, bali wanaendelea na tabia hiyo hiyo, tena kwa kibri na kejeli, ambayo itatusababisha tena kuwaonyesha

makosa ya Shekhe wao Hajuri kama tutakavyoona hapo mbele, ili waelewe kua kama wanamhukumu Fulani kua mjinga kwa kukosea vitu kama hivyo, basi wamhukumu skhekhe wao pia ambaye amekosea kwenye makubwa zaidi ya hayo!

Miongoni mwa mifano ya kushangaza; ni Khamis Ame alipochukua muda mrefu kukejeli, na kutukana kwamba mjinga, mwenda wazimu, na kuonyesha dharau za kila aina, kwa sababu tu ya kukosea kumtaja swahaba radhi za Alla zimuendee!

Ambapo usahihi riwaya Imepokewa na Hudhaifa Ibn Al yamaany Radhi za Alla zimuendee(kama nilivyobainisha kwenye makala iliyopita), lakini nikateleza nikasema ni ya Nu'uman bin Bashiir Radhi za Alla zimuendee.

Kwa hakika hii ndio manhaji waliyokemea wanachuoni, hivi mtu akighafilika kwa bahati mbaya akakosea kumtaja swahaba ndio mjinga? Ndio hana akili? Ndio anadharauliwa?

Yani Khamis Ame anataka kusema yeye hakosei? Yeye haghafiliki? Ikiwa yeye hakosei makosa kama

haya imma kwa kughafilika au kuteleza ulimi: basi Maashaa Alla, atakua yeye katimia! Na ni mwanachuoni mkubwa sana asiye na mfano hapa duniani!

Halafu ewe unayeona kua kukosea jina la mpokezi wa hadithi ni ujinga, je, utakubali tutakapoleta makosa ya Hajuri yaliowazi zaidi ya hayo umuite mjinga? Asiye na akili?

Pamoja na hivyo, baada ya kugundua baadhi ya hizi auhaam, na kwa kupitia mtandao wa whatshap, nilitoa tanbihi ya hili kosa na mengineyo kwenye grp ya kisalafy Tar 15/8/2016 saa tano na dakika ishirini na tisa usiku, kwenye grp liitwalo الدعوة السلفية في تنزانيا kama nilivyobainisha kwenye makala iliyopita.

Ambapo baada ya hapo, ndio Khamis Ame akatoa kejeli yake na dharau zake tulizotaja hapo juu.

Pia miongoni mwa mifano hiyo: ni pale Khamis Ame alipotoa kejeli, na dharau, na matusi, kwa sababu nimekosea lafdhi ya hadithi ambapo badala ya

kusema:على ثلاث وسبعين فرقةNilisema:إلى ثلاثة وسبعين فرقة

kwa mujibu wa Khamis Ame, anayekosea lafdhi ya Hadithi, au kukosea mpokezi wa hadithi, au kukosea Aya na nk ni mjinga, hana elimu, ni feki mgonjwa na nk:

JE NI VIPI MASHEKHE WAKE WALIOKOSEA MAKOSA ZAIDI YA HAYA ANAWAHUKUMU HUKMU SAWA?

Kwa hakika ndugu msomaji hapa ndipo tutaona uadilifu wa Khamis Ame, je nao atawaita majahili? Atawabeza? Au hili ni makhsusi tu kwa mtu maalumu kutokana na msukumo maalumu uliojawa na chuki pamoja na husda zilizojificha?

Na kabla ya kuaona mifano ya makosa ya mashekhe wao wakubwa: ningependa tuone moja miongoni mwa makosa aliyoingia Abdurra'hman katika huo huo mhadhara wake wa kunikosoa, ambapo alinukuu hadithi akasema kama ninavyomnukuu:

"(inatosha pale ambapo mtume swalla llaahu alaihi wasallam ameifaradhisha ilimu kwa umma wake,

طلب العلم فريضة على كل مسلم ومسلمة

Kwamba kutafuta ilimu, ni fardhi juu ya kila muislamu mwana mume, na muislamu mwanamke)"

mwisho wa kunukuu.

Nadhani unashuhudia mwenyewe ndugu msomaji, jinsi Abdrurrah'man alivyoinukuu hadithi hii, Ambapo tunaona kua Abdurra'man kaisoma hadithi na kuzidisha lafdhi ambayo haimo, nayo ni neno:

ومسلمة

Neno hili halipo kwenye hadithi, bali limeongezwa na waandika vitabu: amesema mwanachuoni wa hadithi Assakhaawy Alla amrehemu–alipokua akiielezea hadithi hiyo–:"

"ألحق بعض المصنفين بآخر هذا الحديث (ومسلمة) وليس لها ذكر في شيء من طرقه وإن كان معناها صحيحا"

المقاصد الحسنة ص: ٤٤٢.

"Baadhi ya waandika vitabu wameingiza mwisho wa hadithi ya" طلب العلم فريضة على كل مسلم " neno " ومسلمة ", na neno hili halijatajwa kabisa kwenye njia za hadithi hii, japo maana yake ni sahihi"

Tazama: maqaaswidul hasanah uk:442.

Kwa hiyo neno hilo alilozidisha Abdrurrah'man halimo, na mimi siwezi kumkejeli Abdurrah'man kwa kosa kama hili, kwakua ninafahamu kua huku ni kuteleza kwa kawaida tu ambako wakati mwingine hutokea bila kukusudia.

Lakini kwa manhaji ya Khamis Ame, Inamlazimu amuite huyu mwenzake mjinga, na amkejeli na kumdharau! Jambo ambalo hawezi, kwakua ni mwenzake!

Na kwa faida tu ni kua hadithi hiyo hata bila hilo neno lilozidi ambalo halimo kabisa, ina khilafu kati ya wanachuoni wa hadithi, wako walioisahihisha, na wako walioidhoofisha. Hii ni kwa faida tu.

BAADA YA KUONA MFANO HUO: SASA TUONE MFANO MWINGINE, wa shekhe wao Yahja Al Hajuury:

Yahaya Al hajuri pamoja na kua yeye ndio shekhe wao mkubwa, na wanamuita Al Allaamah, na mengineyo katika majina ya sifa: lakini kuna makosa mengi sana ambayo msomaji hawezi amini kirahisi kua haya ni makosa yake!

Nitaorodhesha baadhi ya makosa yake yaliothibiti kwenye vitabu vyake na darasa zake!

MIONGONI mwa makosa hayo ni haya yafuatayo:

1- katika kaseti iitwayo:

التنبيه النفيس على أخطاء حدثت في جلسة الوالد الرئيس

Yahya Al Hajuury alipokua anajibu kauli isemayo:

كل مجتهد مصيب

" kila mwenye kujitahidi anapatia" KASEMA:

حتى النصارى يجتهدون في أن الله ثالث ثلاثة فهل هم مصيبون؟ لا

" Hata manaswara(wakiristo) wanajitahidi katika kusema kwao waungu wako watatu, je wamepatia? Hapana"

mwisho wa kunukuu.

Hakika khamis Ame kosa kama hili ndilo hasa unahitajika umkejeli Shekhe wako na kumpa sifa ulizowapa wengine kwa Dhulma, na uthibitishe kua hana elimu, na wala usikejeli aliyekosea kwa bahati

mbaya kutamka jina la swahaba, au aliyeteleza kwa bahati mbaya katika kuisoma Aya au lafdhi ya hadithi au ibara ya kiarabu.

.

Kwani kwa hakika anayesema Wakiristo wamejitahidi kudai kua kuna waungu watatu lakini wakakosea: huyu anahitaji akaziwe maneno na akemewe vikali kwa kauli hiyo ambayo ni kufru!, jambo ambalo kwa masikitiko huwezi kulifanya!

Hivi ni muislamu gani – hata kichaa– leo hii atasema: wakiristo kusema kwao waungu ni watatu wamejitahidi wakakosea kama vile kujitahidi kwa wanachuoni kwenye maswala ya kifiqhi wakakosea?

2– Katika kaseti mojawapo ya Yahya Al hajuury iitwayo:

أسئلة أصحاب يامي

Katika moja ya maswali aliyoulizwa Hajuri kwenye kaseti hii, ni kuhusu ubeti wa Al buuswiiry wa kishirki usemao:

" يا أكرم الخلق ما لي من ألوذ به سواك عند حدوث الحادث العمم"

Ambapo Hajuri alijibu kuhusu kipengele cha

kwanza akasema:

" يا أكرم الخلق: هذه الفقرة صواب"

"ewe mkarimu zaidi wa viumbe:(kipande hiki) ni sahihi".

Ni makosa makubwa sana Hajuri kusema kipande hicho cha Ubeti kiko sahihi, kwani hakuna shaka kua Mtume Swalla Llaahu Alaihi wasallam ni mmbora wa viumbe, na ni mkarimu zaidi ya viumbe wote:

lakini huo ubeti hapo umekuja katika njia ya kufanya istighatha(kutaka msaada) kwa Mtume, na hii ni Shirki kubwa inayomtoa mtu kwenye Uislamu!

Sasa vipi Hajuri aseme kipande hicho ni sahihi? Wakati anaona wazi kua huo ubeti ni wa kutaka msaada kwa Mtume? Kama walivyobainisha wanachuoni akiwemo Ibnu Baazi Allah amrehemu? Sasa Hajuri atawekwa daraja gani na Ame?

Hayo mawili ni mifano michache sana ya makosa ya Hajuri ambayo mengine ni ya kumtoa kwenye Sunna kabisa, bali baadhi yake ni Kufru!

Na pia kuna makosa mengine ya kiitikadi ambayo ni maarufu kwa wengi ambayo Hajuri ameyafanya, kama vile kudai yafuatayo:

1- kua swahaba Oth'man Radhi za Alla zimuendee amezusha Bida'a ya Adhana! na hakuna shaka kua huu ni uongo wa wazi kabisa! Kwani usahihi ni kua Adhana ya Othmaan Radhi za Alla zimuendee ni Sunna na si bida'a, kama walivyobainisha wanachuoni.

2- amesema: Baadhi ya maswahaba walishiriki kumuua Swahaba na Khalifa wa Tatu Oth'man Bin Affaan Radhi za Allla zimuendee, na hakuna shaka kua hii sio sahihi, na hakuna hata swahaba mmoja aliyeshiriki kumuua Othman Radhi za Alla zimuendee.

Na kwa kujua kua ni kweli alikosea: kwenye chapa zingine za kitabu chake aliondosha hiyo Ibara kimya kimya(bila kubainisha kua alikosea na kutoa bayani)!

3- pia amesema Hajuri: Bida'a ya Irjaa'a imezushwa na Swahaba O'thman bin Madh'uun Radhi za Alla zimuendee, kisha akanasibisha maneno hayo na Ibnu Taimiyya Allah amrehemu.

Na kwa hakika huku ni kumsingizia Ibnu Taimiyya, kwani hakuna sehemu ambayo Imaam Ibnu Taimiyya amesema hayo, pia hakuna sehemu hata moja katika vitabu vya Ahlussunna inayosema kuna swahaba kaanzisha bida'a, bali wanaowatuhumu maswahaba ni maraafidhwa na makhawariji!

Hayo ni baadhi ya makosa ya Hajury ambayo hatuwezi kuyamaliza kuyataja yote hapa, na yanaonyesha wazi jinsi Shekhe wenu mkubwa ambaye kwenu ni Al allaama alivyokosea kwenye mambo ya hatari sana!

Sasa na yeye ataitwa mjinga na Khamis Ame? Je ataambiwa mgojwa? Au hilo la kutukanwa hayo ni kwa Ajili ya aliyekosea lafdhi ya hadithi huku maana ikiwa sahihi? Au ni kwa ajili ya aliyekosea jina la

mpokezi wa Hadithi?

Lakini kabla ya kumaliza: nimuonyeshe Ame makosa ya Shekhe wao mwingine mkubwa anayeitwa Abdul Hamiid Al hajuury ya kilunga na kiuandishi , ambapo tutaona makosa yake na inavyotakiwa iwe, hususan katika kitabu chake kiitwacho:

" الخيانة الدعوية"

kabla hajarekebisha baadhi ya makosa hayo kimya kimya kwenye chapa zingine baada ya kubainishwa makosa hayo na baadhi ya mashekhe wa kisunna.

baadhi ya mifano ya makosa aliyokosea kwenye kitabu hicho mwanzo na kukosolewa ni kama ifuatavyo:

Gamba la juu kabisa aliandika:

قرأه وقدم له : الشيخ العلامة المحدث أبي!! عبدالرحمن

sahihi ni:

أبو

Uk:72 aliandika:

وللعلم أن لهم طرق! عديدة

sahihi ni:

طرقا

Uk:81 aliandika:

لكنهم عن الحق معرضين! ، ولسبيل الشيطان سالكين

sahihi ni:

سالكون ، معرضون

Uk: 81 aliandika:

وخان عقيل ...شيخنا مقبل! رحمه الله

Sahihi ni:

مقبلا

Uk: 82 aliandika:

قاد لوائها

sahihi ni:

لواءها

Uk: 83 aliandika:

فلا تكن يا عبد الله سبب! لتفريق وحدة الصف

Sahihi ni:

سببا

Uk:83 aliandika:

إذا رأيت رجل! في السماء

sahihi ni:

رجلا

Uk:89 aliandika:

فأهل السنة مناصرين! للحق

sahihi ni:

مناصرون

Uk: 92 aliandika:

وللشيخ ربيع ردوداً! عليه "

sahihi ni:

ردود

Uk: 96 aliandika:

فجعلوا مخالفة القرآن والإعراض عنه سبب!! للغلبة

sahihi:

سببا

Uk: 98 aliandika:

وقال تعالى مبينا أنه ممكنا

sahihi ni:

ممكن

Uk:99 aliandika:

فإذا كان المؤمن مأمور! بأداء الأمانة

sahihi ni:

مأمورا

Haya ni baadhi tu ya makosa ambayo yalikua kwenye kitabu chicho cha Abdul Hamid Al Hajuury, ambaye kwenu yeye ni katika mashekhe wakubwa sana wa kutegemewa!

Sasa sijui kwa makosa haya Khamis Ame atamuambia maneno gani? Atamuambia jaahili? Au mgonjwa? Au shekhe feki?

Na ukiangalia kwa makini hayo makosa, basi utaona kinachomsumbua Allaama wenu, ni Ismu Inna na Khabari yake, pia Ismu kaana na Khabari yake, yani mlango huu inaelekea unampa shida sana!.

Na kushauri Khamis Ame siku nyingine ujifunze kukosoa kwa adabu na heshima kwenye vitu ambavyo tullaabul Ilmi wanajua kua hivi ni vitu vya kawaida ambavyo unatakikana utaje usahihi wake tu kisha unaendelea bila kukejeli wala kushupalia.

Kwani ikiwa utaendeleza mtindo huu, basi elewa kua wengine pia watayatoa makosa kama hayo tena na makubwa zaidi yaliyoko kwako na mashekhe zako kama tulivyoona hapo!

Na hayo makosa ya ki Imla na kilugha tuliyotaja hapo lengo si lingine, bali nikumuonyesha Ame kua makosa kama haya yanapatikana kwa wingi sana kwa

mashekhe zako, na si kwa lengo la udhalilishaji!

Na kufikia makala hii: tunaweka kituo kwanza mpaka hapo itakapohitajika kubainisha makosa mengine tena Inshaa Allah kulingana na nafasi na umuhimu wa kinachotakikana kubainishwa.

kwani si kila kinachozungumzwa chajibiwa, na si kila anayezungumza apatilizwa.

IMEANDIKWA NA:

ABUU IBRAAHIIM IBNU AL IMAAM.

وفقه الله وغفر له ولوالديه ولجميع المسلمين.

١٤٣٨/٤/٢٢هـ